

*Kumb.Na. C/AB/10/48/01*

24 Januari, 2002

**REKEBISHO A: KWA WARAKA WA UTUMISHI NA. 1  
WA MWAKA 1999**

Tarehe ya kuanza kutumika 19 Machi, 1999.

Baada ya Ibara ya 3.5 ongeza Ibara nyingine 3.6 na isomeke kama ifuatavyo:—

3.6.1. Utaratibu wa ajira za Watumishi wote waliotoka Serikalini utakuwa kama ifuatavyo:

- (i) Watendaji Wakuu ambao walitoka Serikalini hawatajiriwa kwa Mkataba bali watahamishiwa moja kwa moja kwenye Wakala na wataendelea kuchangia kwenye Mfuko wa Pensheni ya Utumishi wa Umma; kwa sababu Sheria ya Mfuko huo inahusu pia Watumishi wa Wakala.
- (ii) Watumishi wengine wote waliotoka Serikalini waliokuwa kwenye Masharti ya Kudumu na Pensheni hao wataendelea na masharti hayo na kuchangia kwenye Mfuko wa Pensheni ya Utumishi wa Umma.
- (iii) Mtendaji Mkuu aliyetoka Serikalini atapewa Madaraka ya kuwa Kiongozi kwa kipindi cha miaka mitano (5) akishindwa ataondolewa katika kazi hiyo kwa kutumia utaratibu ulioelezwa katika "Executive Agencies (Personnel Management) Regulation part III "Kifungu cha 7 (1-3).

3.6.2 Baada ya Marekebisho haya Mikataba ya ajira irekebishwe kwa kuzingatia Sheria zilizopo.

3.6.3 Kwa wale ambao michango yao ya Pensheni ilikuwa haipelekwi kwenye Mfuko wa Pensheni baada ya kujiunga na Wakala inabidi Mwajiri apeleke michango yote tangu mtumishi alipohamia kwenye Wakala husika ili mwendelezo uwepo kwenye Utumishi wake.

J. A. RUGUMYAMHETO,  
*Katibu Mkuu (Utumishi).*